


Muhtasari wa Mkutano



Ahadi za Maagano

Rais Oaks alifundisha kwamba agano ni ahadi ya kufanya mambo fulani. Kwa mfano, madaktari na zima moto wanafanya agano la kuwasaidia watu katika jumua zao. Tunapofanya maagano na Baba yetu wa mbinguni, kama vile tunapobatizwa, tunaahidi kumtumikia Yeye na kuzitii amri Zake. Yeye anatubariki sisi tunaposhika maagano yetu.


Hii inanifundisha:



Endelea kupiga makasia.

Mzee Renlund alisimulia kuhusu safari kwa kutumia mtumbwi wa Kieskimo ambapo alipiga kasia mbele zaidi ya familia yake. Aliposimama, wimbi lilimwangusha ndani ya maji. Mwongozaji alimwambia aendelee kupiga kasia ili asonge mbele na asianguke. Kama tukiendelea "kupiga kasia" kuelekea kwa Mwokozi, tunaweza kuwa salama na kulindwa.

Hii inanifundisha:



Kupata Ushuhuda

Rais Pace alishiriki jinsi gani wakati alipokuwa na umri wa miaka 11, mama yake alimuuliza kama yeye binafsi alifahamu kwamba injili ni ya kweli. Aliamua kusoma Kitabu cha Mormoni na kusali ili apate kujua. Kadiri alivyofanya, alijisikia faraja na amani kutoka kwa Roho Mtakatifu. Hii ilimsaidia yeye kupata ushuhuda wake mwenyewe.

Hii inanifundisha:



Mawe matano

Dada Spannaus alisimulia hadithi ya Daudi na Goliathi. Kama vile Daudi alivyokuwa na mawe matano ili kupigana na Goliathi, yapo mawe "matano" ya kukusaidia wewe ukabiliane na changamoto katika maisha. Haya ni upendo kwa Mungu, imani katika Yesu Kristo, kujua kwamba wewe ni mwana wa Mungu, toba ya kila siku, na ufikiaji kwenye nguvu ya Mungu.

Hii inanifundisha:

